HOTUBA YA MHESHIMIWA JAKAYA MRISHO KIKWETE RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA HAFLA YA UZINDUZI RASMI WA UJENZI WA BARABARA YA TANGA – HOROHORO KWA KIWANGO CHA LAMI, TAREHE 28 MEI 2010.

Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa (Mb), Waziri wa Miundombinu,

Waheshimiwa Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mheshimiwa Meja Jenerali Mstaafu Said Kalembo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga,

Mheshimiwa Alfonso E. Lenhardt, Balozi wa Marekani nchini,

Mheshimiwa Daniel W. Yohannes, Rais wa Mfuko wa Changamoto za Millenia (MCC)

Waheshimiwa mabalozi,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,

Waheshimiwa Wabunge,

Wageni Waalikwa,

Ndugu Wananchi,

Mabibi na Mabwana.

1. Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha wageni wote mliokuja kujumuika nasi katika uzinduzi rasmi wa ujenzi wa barabara ya Tanga - Horohoro.

Kwa nafasi ya kipekee, napenda kuwakaribisha Balozi wa Marekani nchini mwetu Balozi Alfonso Lenhardt na Rais wa *Millennium Challenge Corporation* (MCC) Mheshimiwa Daniel W. Yohannes aliyesafiri kutoka Washington D.C. Marekani, kuja kujumuika nasi katika uzinduzi huu.

Ndugu Wananchi,

2. Barabara hii inajengwa kwa fedha za msaada kutoka Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Changamoto ya Milenia. Mwezi Februari mwaka 2008, nilisaini makubaliano ya msaada wa dola za Kimarekani karibia milioni 700 kutoka Serikali ya Marekani kugharamia miradi ya kuimarisha baadhi ya miundombinu ya barabara, umeme na maji.

Miradi ya barabara iliyo katika mpango huu ni;

i) Barabara ya Tanga – Horohoro

ii) Barabara ya Tunduma – Sumbawanga

iii) Barabara mbili katika ukanda wa Mtwara ambazo ni Peramiho - Mbinga na Songea hadi Namtumbo

iv) Barabara tano za vijijini katika kisiwa cha Pemba na

v) Upanuzi wa kiwanja cha ndege katika kisiwa cha Mafia.

Miradi ya umeme ni;

i) Mradi wa kupeleka umeme Zanzibar (katika kisiwa cha Unguja) kutoka katika gridi ya Taifa kupitia chini ya bahari

ii) Uimarishaji na upanuzi wa mtandao wa umeme katika mikoa sita ya Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya, Dodoma na Mwanza,na

iii) mradi wa umeme wa maji kutoka mto Malagarasi na uimarishaji wa mtandao wa umeme Kigoma.

Miradi ya maji ni;

i) upanuzi wa mitambo wa kuchuja maji wa Ruvu chini kwa ajili ya jiji la Dar es Salaam,

ii) ukarabati wa mfumo wa maji kwa mji wa Morogoro na mradi wa kupunguza maji yasiyolipiwa kwa jiji la Dar es Salaam na Bagamoyo.

Maandalizi ya miradi hii yanaendelea vizuri na mikataba yote ya kazi za ujenzi inategemewa kusainiwa mwaka huu. Nyote mtakubaliana nami kuwa hizi si fedha kidogo.

Napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuishukuru kwa dhati Serikali ya Marekani kwa msaada huu mkubwa. Napenda niihakikishie Serikali ya Marekani kupitia kwa Mheshimiwa Balozi Alfonso E. Lenhardt na Rais wa *Millenium Challenge Corporation* Mheshimiwa Daniel W. Yohannes, kwamba Wananchi wa Tanzania tunathamini sana michango yao na tunawashukuru sana .

Ndugu Wananchi,

3. Tulichagua ujenzi wa miundo mbinu kwa kutambua umuhimu na mchango mkubwa wa sekta hii katika kukuza uchumi na kuimarisha harakati za kuondokana na umaskini. Kikwazo kikubwa katika jitihada za kuvutia wawekezaji wa ndani na nje, na hivyo kuongeza ajira na kipato kwa wananchi, ni upungufu au kukosekana kwa miundo mbinu muhimu ya barabara na mawasiliano, umeme na maji. Hivyo jitihada za kuimarisha miundo mbinu zinalenga kuongeza shughuli za kiuchumi ambapo matokeo yake ni ongezeko la ajira na kipato, uboreshaji wa maisha na kupungua kwa umaskini.

Ndugu Wananchi,

4. Tuliahidi maisha bora kwa kila Mtanzania, lakini maisha bora hayapatikani kwa miujiza. Maisha bora yanapatikana kwa kuongezeka kwa ajira na kipato, kuongeza uzalishaji na kufikisha mazao sokoni na hivyo kupata mapato zaidi na kupatikana kwa huduma muhimu kwa urahisi. Vyote hivi vinategemea sana uimarishaji wa miundombinu. Miradi yote inayofadhiliwa na MCC ikijumuisha huu wa Barabara ya Tanga – Hororo tunauouzindua leo, imejikita katika eneo hili muhimu la kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Ndugu Wananchi,

5. Kama alivyotangulia kusema Waziri wa Miundombinu, uimarishaji wa mtandao wa barabara unafanyika wakati tunaimarisha ushirikiano wa nchi zetu za Afrika Mashariki. Barabara hii ina umuhimu mkubwa kwa nchi yetu na majirani zetu pia. Inaunganisha mitandao ya barabara kutoka kusini na kati ya Tanzania na mitandao ya barabara za Kenya kupitia Mji wa mpakani wa Horohoro na bandari ya Mombasa. Hivyo ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami utasaidia kukuza biashara kati yetu na nchi jirani ya Kenya. Natoa wito kwa Watanzania kuchangamkia fursa za kibiashara zinazoendelea kuongezeka. Tusipofanya hivyo tutajikuta tunawanufaisha wenzetu na sisi kubaki wasindikizaji.

Ndugu Wananchi,

5. Kuna vitendo vingi, tena vya aibu, vinavyofanywa na baadhi ya wananchi kinyume na juhudi za Serikali za kuboresha mtandao wa barabara zetu, ambavyo vinachangia kuturudisha nyuma. Waziri wa Miundo Mbinu amezungumzia udokozi unaofanywa na baadhi ya Wananchi wachache. Hivi ni vitendo vya aibu ambavyo haviwezi kuvumiliwa na Serikali. Wizi wa mafuta, vipuri vya mitambo na magari yanayotumika na Mkandarasi katika ujenzi, Wizi wa Saruji, Mbao, Nondo nk. Vitendo hivi kwa hakika vinachangia kuzorotesha kazi za ujenzi na wakati mwingine kusababisha ongezeko la gharama za ujenzi na

hatimaye kupunguza tija na ufanisi wa ubora wa kazi. Tabia hii iachwe kabisa. Naziagiza taasisi za Serikali, kila moja kwa nafasi yake kuhakikisha kuwa hatua za kisheria zinachukuliwa kwa wote watakaojihusisha na vitendo hivi.

Ndugu Wananchi,

6. Tusisahau kuhusu balaa la UKIMWI. Tumelizungumza mara nyingi kiasi kuwa imekuwa kama wimbo lakini kwa sababu ni tatizo linaloathiri jamii yetu tutaendelea kulipigia kelele. Ujenzi wa barabara una kawaida ya kuwaleta pamoja wafanyakazi kutoka maeneo tofauti. Aidha, shughuli za kijamii na kiuchumi zitaongezeka kwa kipindi chote cha ujenzi. Kwa bahati mbaya, mkusanyiko wa watu unachangia ongezeko la maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi. Napenda nitoe wito kwa Watanzania wenzangu tujiepushe na vitendo au mazingira yanayoweza kuchangia maambukizi ya ugonjwa huu hatari usiokuwa na kinga wala tiba. Hatupendi baada ya ujenzi kukamilika tuwe na ongezeko la maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Tuchukue tahadhari.

Waheshimiwa Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Kwa furaha kubwa sasa nachukua nafasi hii kuzindua rasmi ujenzi wa barabara ya Tanga – Horohoro inayojengwa kwa kiwango cha lami.

AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.